

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam **Mhe. Paul C. Makonda** amekabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani **Mhe. Mhandisi Evarist Ndikilo** mapema leo asubuhi baada ya kukaa ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam kwa muda wa **siku tano** kuanzia tarehe **27/05/2017** mpaka tarehe **31/05/2017**

Makabidhiano hayo yamefanyika katika Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere Terminal One na kuhudhuriwa na Viongozi mbalimbali wakiwemo Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam, Viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Wahe. Madiwani, Wakurugenzi wa Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam, Makatibu Tawala wa Wilaya zote, Wadau mbalimbali wa Maendeleo, Watumishi wa Sekretarieti ya Mkoa na Vikundi vya Hamasa vya Mkoa wa Dar es Salaam.

Awali, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alianza kwa kumshukuru Mungu na kuwakaribisha wote waliofika kwa ajili ya tukio muhimu la makabidhiano ya Mwenge wa Uhuru.

Katika hotuba yake **Mhe. Paul Makonda** alieleza jinsi Mwenge wa Uhuru ulivyotimiza azma yake kwa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kukagua miradi yenye thamani ya Tshs **244,392,530,334/=** ambapo miradi **mikubwa 12 ilizinduliwa, miradi 5 iliwekewa mawe ya msingi, na miradi 11 ilitembelewa na kufunguliwa.**

Mhe. Paul Makonda alieleza kuwa aliupokea Mwenge wa Uhuru ukitokea katika Mkoa wa Lindi na umefanya mambo mengi makubwa na mazuri kwa Wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam, hivyo amekabidhi Mwenge huo kwa

Mkoa wa Pwani kwa moyo mweupe ili ukazindue, kutembelea na kuweka Mawe ya Msingi katika Miradi mbalimbali Mkoani humo.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Pwani **Mhe. Mhandisi Evarist Ndikilo** amesema kuwa ameupokea Mwenge wa Uhuru na akiahidi kuukimbiza katika katika Wilaya zote saba zilizopo katika Mkoa huo sambamba na kuzindua, kutembelea na kuweka Mawe ya Msingi katika Miradi itakayogharimu zaidi ya Shilingi Bilioni themanini na tano.

Mbio za Mwenge wa Uhuru katika Mkoa wa Dar es Salaam zimekua kichocheo kikubwa katika kuhamasisha Maendeleo, Uzalendo, Umoja, Mshikamano na Kudumisha Amani.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

01/06/2017